

Jinsi ya kutengeneza Mkate wa mayai

By SW - Melkisedeck Shine · April 9, 2022

Dondoo za Mapishi na Lishe · Upishi na Maandalizi ya Milo yenye Afya · #Karibu AckySHINE

Mahitaji

Slice za mkate 6 Mayai 3 Chumvi Olive oil

Matayarisho

Vunja mayai yote katika sahani kisha tia chumvi kidogo sana na uyapige mpaka chumvi ichanganyike. Kisha chukua frying pan na utie vimafuta kidogo na uweke jikoni. Mafuta yakishapata moto kiasi, chovya slice za mkate katika hayo mayai na uzipike pande zote zikishaiva zitoa na uziweke katika kitchen towel ili kukausha mafuta. Na baada ya hapo mikate yako itakuwa tayari kwa kuliwa na chai.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=24672>